# Zekaria

### *Wito wa kumrudia Mwenyezi Mungu*

1 Katika mwezi wa nane wa mwaka wa pili
wa utawala wa Dario, neno la Mwenyezi Mungu
lilimjia nabii Zekaria mwana wa Berekia, mwana
wa Ido, kusema:
2 “Mwenyezi Mungu aliwakasirikia sana baba
zako wa zamani.
3 Kwa hiyo waambie watu: Hili ndilo asemalo
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbin-
guni: ‘Nirudieni mimi,’ asema Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni, ‘nami nitawaru-
dia ninyi,’ asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni.
4 Msiwe kama baba zenu, ambao manabii
waliotangulia waliwatangazia: Hili ndilo ase-
malo Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni: ‘Geukeni, mziache njia zenu mbaya na
matendo yenu maovu.’ Lakini hawakunisikiliza
wala kufuata maelekezo yangu, asema Mwenyezi
Mungu.
5 Wako wapi baba zako sasa? Nao manabii, je,
wanaishi milele?
6 Je, maneno yangu na amri zangu nilizowaa-
giza manabii watumishi wangu, hayakuwapata
baba zenu?

“Kisha walitubu na kusema, ‘Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni ametutenda sawasawa na njia zetu na matendo yetu yalivyostahili, kama alivyokusudia kufanya.’ ”

### *Maono ya kwanza: Mtu katikati ya miti ya mihadasi*

7 Katika siku ya ishirini na nne ya mwezi wa kumi na moja, yaani mwezi uitwao Shebati, katika mwaka wa pili wa utawala wa Dario, neno la Mwenyezi Mungu lilimjia nabii Zekaria mwana wa Berekia mwana wa Ido.

8 Wakati wa usiku nilipata maono, na tazama, mbele yangu palikuwa na mtu akiendesha farasi mwekundu! Alikuwa amesimama katikati ya miti ya mihadasi kwenye bonde. Nyuma yake walikuwepo farasi wekundu, wa kikahawia, na weupe.

9 Nikauliza, “Hivi ni vitu gani bwana wangu?”

Malaika aliyekuwa akizungumza na mimi akanijibu, “Nitakuonesha kuwa ni nini.”

10 Kisha yule mtu aliyesimama katikati ya miti ya mihadasi akaeleza, “Ni wale ambao Mwenyezi Mungu amewatuma waende duniani kote.”

11 Nao wakatoa taarifa kwa yule malaika wa Mwenyezi Mungu, aliyekuwa amesimama katikati ya miti ya mihadasi, “Tumepita duniani kote na kukuta ulimwengu wote umepumzika kwa amani.”

12 Kisha malaika wa Mwenyezi Mungu akasema, “Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni, utazuia hadi lini rehema kutoka Yerusalemu na miji ya Yuda, ambayo umeikasirikia kwa miaka hii sabini?”

13 Kwa hiyo Mwenyezi Mungu akazungumza maneno ya upole na ya kufariji kwa malaika aliyezungumza nami.

14 Kisha malaika yule aliyekuwa akizungumza
nami akasema, “Tangaza neno hili: Hili ndilo
asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi
ya mbinguni: ‘Nina wivu sana kwa ajili ya
Yerusalemu na Sayuni,
15 lakini nimeyakasirikia sana mataifa yanay-
ojisikia kuwa yako salama. Nilikuwa nime-
wakasirikia Israeli kidogo tu, lakini mataifa hayo
yaliwazidishia maafa.’
16 “Kwa hiyo, hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi
Mungu: ‘Nitairudia Yerusalemu kwa rehema
na huko nyumba yangu itajengwa tena.
Nayo kamba ya kupimia itanyooshwa juu ya
Yerusalemu,’ asema Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni.
17 “Endelea kutangaza zaidi kwamba: Hivi
ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni: ‘Miji yangu itafurika
tena ustawi na Mwenyezi Mungu atamfariji tena
Sayuni na kumchagua Yerusalemu.’ ”

### *Maono ya pili: Pembe nne na mafundi wanne*

18 Kisha nikatazama juu, na pale mbele yangu
nikaona pembe nne!
19 Nikamuuliza yule malaika aliyekuwa ak-
izungumza nami, “Ni nini hizi?”

Akanijibu, “Hizi ni zile pembe zilizowatawanya
Yuda, Israeli na Yerusalemu.”
20 Kisha Mwenyezi Mungu akanionesha ma-
fundi wanne.
21 Nikauliza, “Hawa wanakuja kufanya nini?”

Akanijibu, “Hizi ndizo pembe zilizowatawanya
Yuda ili asiwepo atakayeweza kuinua kichwa

chake, lakini mafundi wamekuja kuzitia hofu na kuzitupa chini hizi pembe za mataifa ambayo yaliinua pembe zao dhidi ya nchi ya Yuda na kuwatawanya watu wake.”

# 2

*Maono ya tatu: Mtu mwenye kamba ya kupimia*

1 Kisha nikatazama juu: pale mbele yangu palikuwa na mtu mwenye kamba ya kupimia mkononi mwake!
2 Nikamuuliza, “Unaenda wapi?”

Akanijibu, “Kupima Yerusalemu, kupata urefu na upana wake.”

3 Kisha malaika aliyekuwa akizungumza nami akaondoka, malaika mwingine akaja kukutana naye
4 na kumwambia: “Kimbia, umwambie yule kijana, ‘Yerusalemu utakuwa mji usio na kuta kwa sababu ya wingi wa watu na mifugo iliyomo.
5 Mimi mwenyewe nitakuwa ukuta wa moto kuuzunguka,’ asema Mwenyezi Mungu, ‘nami nitakuwa utukufu wake ndani yake.’

6 “Njooni! Njooni! Kimbieni mtoke katika nchi ya kaskazini,” asema Mwenyezi Mungu, “kwa kuwa nimewatawanya kwenye pande nne za mbingu,” asema Mwenyezi Mungu.

7 “Njoo, ee Sayuni! Kimbia, wewe ukaaye ndani ya Binti Babeli!”

8 Kwa kuwa hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni: “Baada ya yeye kuniheshimu na kunituma mimi dhidi

ya mataifa yaliyokuteka nyara, kwa kuwa yeyote awagusaye ninyi, anaigusa mboni ya jicho lake,
9 hakika nitauinua mkono wangu dhidi yao ili watumwa wao wawateke nyara. Ndipo mtajua kuwa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni amenituma.
10 “Shangilia na ufurahie, ee Binti Sayuni, kwa maana ninakuja, nami nitaishi miongoni mwenu,” asema Mwenyezi Mungu.
11 “Mataifa mengi yataunganishwa na Mwenyezi Mungu siku hiyo, nao watakuwa watu wangu. Nitaishi miongoni mwenu, nanyi mtajua kuwa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni amenituma kwenu.
12 Mwenyezi Mungu atairithi Yuda kama fungu lake katika nchi takatifu na atachagua tena Yerusalemu.
13 Tulieni mbele za Mwenyezi Mungu, enyi watu wote, kwa sababu ameinuka kutoka makao yake matakatifu.”

# 3

## *Maono ya nne: Mavazi safi kwa ajili ya kuhani mkuu*

1 Kisha akanionesha Yoshua*, kuhani mkuu, akiwa amesimama mbele ya malaika wa Mwenyezi Mungu, naye Shetani amesimama upande wake wa kuume ili amshtaki.
2 Mwenyezi Mungu akamwambia Shetani, “Mwenyezi Mungu akukemee Shetani! Mwenyezi

* **3:1** Kwa Kiebrania ni *Yeshua*, maana yake *Yehova ni wokovu.*

Mungu, ambaye ameichagua Yerusalemu, akukemee! Je, mtu huyu siyo kijinga kinachowaka kilichonyakuliwa kwenye moto?"

3 Wakati huu, Yoshua alikuwa amevaa nguo
chafu alipokuwa amesimama mbele ya malaika.
4 Malaika akawaambia wale waliokuwa
wamesimama mbele yake, "Mvueni hizo nguo zake chafu."

Kisha akamwambia Yoshua, "Tazama, nimeiondoa dhambi yako, nami nitakuvika mavazi ya kitajiri."

5 Kisha nikasema, "Mvike kilemba kilicho safi
kichwani mwake." Kwa hiyo wakamvika kilemba safi kichwani na kumvika yale mavazi mengine, wakati malaika wa Mwenyezi Mungu akiwa amesimama karibu.
6 Malaika wa Mwenyezi Mungu akamwamuru
Yoshua:
7 "Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni: 'Ikiwa utatembea katika njia zangu na kushika maagizo yangu, basi utaitawala nyumba yangu na kuzilinda nyua zangu, nami nitakupa nafasi miongoni mwa hawa wasimamao hapa.

8 " 'Sikiliza, ee Yoshua kuhani mkuu, pamoja na
wenzako walioketi mbele yako, ambao ni watu walio ishara ya mambo yatakayokuja: Ninaenda kumleta mtumishi wangu, Tawi.
9 Tazama, jiwe nililoliweka mbele ya Yoshua!
Kuna macho saba juu ya jiwe lile moja, nami nitachora maandishi juu yake,' asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni, 'nami nitaiondoa dhambi ya nchi hii kwa siku moja.

10 " 'Katika siku hiyo kila mmoja wenu atamwa-
lika jirani yake akae chini ya mzabibu wake na
mtini wake,' asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni."

# 4

### *Maono ya tano: Kinara cha taa cha dhahabu na mizeituni miwili*

1 Kisha malaika aliyezungumza nami akarudi
na kuniamsha, kama mtu aamshwavyo kutoka
usingizini.

2 Akaniuliza, "Unaona nini?"

Nikajibu, "Ninaona kinara cha taa cha dhahabu tupu, nacho kina bakuli juu yake na taa saba juu yake, tena iko mirija saba ya kuleta mafuta, kwenye taa zote zilizo juu yake.

3 Pia kuna mizeituni miwili karibu yake,
mmoja upande wa kuume wa bakuli na
mwingine upande wa kushoto."

4 Nikamuuliza malaika aliyezungumza nami,
"Hivi ni vitu gani, bwana wangu?"

5 Akanijibu, "Hujui kuwa hivi ni vitu gani?"

Nikajibu, "Hapana, bwana wangu."

6 Kisha akaniambia, "Hili ni neno la Mwenyezi
Mungu kwa Zerubabeli: 'Si kwa uwezo, wala si
kwa nguvu, bali ni kwa Roho wangu Mtakatifu,'
asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni.

7 "Wewe ni kitu gani, ee mlima mkubwa sana?
Mbele ya Zerubabeli wewe utakuwa ardhi tam-
barare. Kisha ataweka jiwe la juu kabisa, na

watu wakishangilia na kusema, ‘Mungu libariki! Mungu libariki!’ ”

8 Kisha neno la Mwenyezi Mungu likanijia:

9 “Mikono ya Zerubabeli iliweka msingi wa Hekalu hili, mikono yake pia italimalizia. Kisha mtajua ya kuwa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni amenituma mimi kwenu.

10 “Ni nani atakayeidharau siku ya mambo madogo? Macho saba ya Mwenyezi Mungu, yanayozunguka dunia yote, yatashangilia yatakapoona jiwe la juu kabisa likiwa mkononi mwa Zerubabeli!”

11 Kisha nikamuuliza yule malaika, “Hii mizeituni miwili iliyo upande wa kuume na wa kushoto wa kinara cha taa ni nini?”

12 Tena nikamuuliza, “Haya matawi mawili ya mizeituni karibu na hiyo mirija miwili ya dhahabu inayomimina mafuta ya dhahabu ni nini?”

13 Akajibu, “Hujui kuwa haya ni nini?”

Nikamjibu, “Hapana, bwana wangu.”

14 Kwa hiyo akasema, “Hawa ni wawili ambao wamepakwa mafuta ili kumtumikia Bwana wa dunia yote.”

# 5

### *Maono ya sita: Kitabu kinachoruka*

1 Nikatazama tena: na hapo mbele yangu kulikuwa na kitabu kinachoruka!

2 Akaniuliza, “Unaona nini?”

Nikamjibu, “Naona kitabu kinachoruka,
chenye urefu wa dhiraa ishirini*, na upana
wa dhiraa kumi†.”
3 Akaniambia, “Hii ni laana inayotoka kwenda
juu ya nchi yote, kwa kuwa kufuatana na yale
yaliyoandikwa katika upande mmoja, kila mwizi
atafukuziwa mbali, pia kufuatana na yaliyo
upande wa pili, kila aapaye kwa uongo ata-
fukuziwa mbali.
4 Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni asema, ‘Nitaituma hiyo laana, nayo
itaingia katika nyumba ya mwizi na nyumba ya
huyo aapaye kwa uongo kwa Jina langu. Itabaki
katika nyumba yake na kuiharibu, pamoja na
mbao zake na mawe yake.’ ”

### *Maono ya saba: Mwanamke ndani ya kikapu*

5 Kisha yule malaika aliyekuwa akizungumza
nami akanijia na kuniambia, “Tazama juu uone
ni nini kile kinachojitokeza.”
6 Nikamuuliza, “Ni kitu gani?”

Akanijibu, “Ni kikapu cha kupimia.” Kisha
akaongeza kusema, “Huu ni uovu wa watu katika
nchi nzima.”
7 Kisha kifuniko kilichotengenezwa kwa
madini ya risasi kilichokuwa kimefunika kile
kikapu, kiliinuliwa na ndani ya kile kikapu
alikuwako mwanamke ameketi!
8 Akasema, “Huu ni uovu,” tena akamsukumia
ndani ya kikapu na kushindilia kifuniko juu ya
mdomo wa kikapu.

---

* **5:2** Dhiraa 20 ni sawa na mita 9. † **5:2** Dhiraa 10 ni sawa mita 4.5.

9 Kisha nikatazama juu: na pale mbele yangu,
palikuwa na wanawake wawili, wakiwa na up-
epo katika mabawa yao! Walikuwa na mabawa
kama ya korongo, nao wakainua kile kikapu na
kuruka nacho kati ya mbingu na nchi.
10 Nikamuuliza yule malaika aliyekuwa ak-
izungumza nami, “Wanakipeleka wapi hicho
kikapu?”
11 Akanijibu, “Wanakipeleka katika nchi ya
Babeli na kujenga nyumba kwa ajili yake.
Itakapokuwa tayari, kikapu kitawekwa pale ma-
hali pake.”

# 6

*Maono ya nane: Magari manne ya vita*

1 Nikatazama juu tena: nikaona mbele yangu
magari manne ya vita yakija kutoka kati ya
milima miwili, milima ya shaba!
2 Gari la kwanza lilivutwa na farasi wekundu,
la pili lilivutwa na farasi weusi,
3 la tatu lilivutwa na farasi weupe, na gari la
nne lilivutwa na farasi wa madoadoa ya kijivu,
wote wenye nguvu.
4 Nikamuuliza malaika aliyekuwa
akizungumza nami, “Hawa ni nani, bwana
wangu?”
5 Malaika akanijibu, “Hizi ni roho nne za mbin-
guni zisimamazo mbele ya uwepo wa Bwana wa
dunia yote, zinatoka kwenda kufanya kazi yake.
6 Gari linalovutwa na farasi weusi linaelekea
katika nchi ya kaskazini, la farasi weupe
linaelekea magharibi, na la farasi wa madoadoa
ya kijivu linaelekea kusini.”

7 Hao farasi wenye nguvu walipokuwa wak-
itoka, walikuwa wakijitahidi kwenda duniani
kote. Akasema, “Nenda duniani kote!” Kwa hiyo
wakaenda duniani kote.
8 Kisha akaniita, “Tazama, wale wanaoenda
kuelekea nchi ya kaskazini wamepumzisha Roho
wangu Mtakatifu katika nchi ya kaskazini.”

### *Taji kwa ajili ya Yoshua*

9 Neno la Mwenyezi Mungu likanijia kusema:
10 “Chukua fedha na dhahabu kutoka kwa watu
waliohamishwa, yaani Heldai, Tobia na Yedaya
ambao wamefika kutoka Babeli. Siku hiyo hiyo
nenda nyumbani mwa Yosia mwana wa Sefania.
11 Chukua fedha na dhahabu utengeneze taji,
nawe uliweke kichwani mwa kuhani mkuu
Yoshua, mwana wa Yehosadaki.
12 Umwambie hili ndilo asemalo Mwenyezi
Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni: ‘Huyu
ndiye mtu anayeitwa Tawi, naye atachipua ku-
toka mahali pake na kujenga Hekalu la Mwenyezi
Mungu.
13 Ni yeye atakayejenga Hekalu la Mwenyezi
Mungu, naye atavikwa utukufu na ataketi ku-
miliki kwenye kiti cha enzi. Atakuwa kuhani
kwenye kiti chake cha enzi. Hapo patakuwa na
amani kati ya hao wawili.’
14 Taji litatolewa kwa Heldai, Tobia, Yedaya
na Heni mwana wa Sefania kama kumbukumbu
ndani ya Hekalu la Mwenyezi Mungu.
15 Wale walio mbali sana watakuja na kusaidia
kulijenga Hekalu la Mwenyezi Mungu, nanyi

mtajua kuwa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni amenituma kwenu. Hili litatokea ikiwa mtamtii Mwenyezi Mungu, Mungu wenu, kwa bidii."

# 7

### *Sio kufunga, bali ni haki na rehema*

1 Katika mwaka wa nne wa utawala wa Mfalme
Dario, neno la Mwenyezi Mungu lilimjia Zekaria
siku ya nne ya mwezi wa tisa, mwezi wa Kisleu.
2 Watu wa Betheli walikuwa wamemtuma
Shareza na Regem-Meleki pamoja na watu wao,
kumsihi Mwenyezi Mungu
3 kwa kuwauliza makuhani wa nyumba ya
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni na manabii, "Je, imempasa kuomboleza na kufunga katika mwezi wa tano, kama ambavyo nimekuwa nikifanya kwa miaka mingi?"

4 Kisha neno la Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni likanijia kusema:
5 "Waulize watu wote wa nchi na makuhani,
'Je, mlipofunga na kuomboleza katika mwezi wa tano na wa saba kwa miaka sabini iliyopita, mlifunga kweli kwa ajili yangu?
6 Na mlipokuwa mkila na kunywa, je,
hamkuwa mnasherehekea kwa ajili ya nafsi zenu?
7 Je, haya sio maneno ya Mwenyezi Mungu
aliyosema kupitia manabii waliotangulia, wakati Yerusalemu pamoja na miji inayoizunguka ilipokuwa katika hali ya utulivu na ya mafanikio,

wakati Negebu na Shefela* zikiwa zimekaliwa
na watu?' "

8 Neno la Mwenyezi Mungu likamjia tena
Zekaria:
9 "Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni: 'Fanyeni
hukumu za haki, onesheni rehema na huruma
ninyi kwa ninyi.
10 Msimdhulumu mjane wala yatima, mgeni
wala maskini. Msiwaziane mabaya mioyoni
mwenu ninyi kwa ninyi.'

11 "Lakini wakakataa kusikiliza, wakanipa
kisogo kwa ukaidi na kuziba masikio yao.
12 Wakaifanya mioyo yao migumu kama
gumegume, na hawakuisikiliza sheria au
maneno ambayo Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni aliyatuma kwa Roho
wake Mtakatifu kupitia manabii waliotangulia.
Kwa hiyo Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi
ya mbinguni, alikasirika sana.

13 " 'Nilipoita, hawakusikiliza; kwa hiyo
walipoita, sikusikiliza,' asema Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni.
14 'Niliwatawanya kwa upepo wa kisulisuli
miongoni mwa mataifa yote, mahali ambapo
walikuwa wageni. Nchi ikaachwa ukiwa nyuma
yao kiasi kwamba hakuna aliyeweza kuingia
au kutoka. Hivi ndivyo walivyoifanya ile nchi
iliyokuwa imependeza kuwa ukiwa.' "

---

* **7:7** au *upande wa magharibi chini ya vilima*

# 8

*Mwenyezi Mungu anaahidi kuibariki Yerusalemu*

1 Neno la Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi
ya mbinguni likanijia tena.
2 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni: "Nina wivu sana kwa
ajili ya Sayuni, ninawaka wivu kwa ajili yake."
3 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu: "Ni-
tarudi Sayuni na kufanya makao Yerusalemu.
Kisha Yerusalemu utaitwa mji wa kweli, mlima
wa Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni utaitwa Mlima Mtakatifu."
4 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni: "Kwa mara nyingine
tena wanaume na wanawake walioshiba umri
wataketi katika barabara za Yerusalemu, kila
mmoja akiwa na mkongojo wake mkononi kwa
sababu ya umri wake.
5 Barabara za mji zitajaa wavulana na wa-
sichana wanaocheza humo."
6 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni: "Mambo haya
yanaweza kuonekana ya ajabu kwa mabaki ya
watu wakati huo, lakini yaweza kuwa ya ajabu
kwangu?" asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni.
7 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni: "Nitawaokoa watu
wangu kutoka nchi za mashariki na magharibi.
8 Nitawarudisha waje kuishi Yerusalemu,
watakuwa watu wangu nami nitakuwa

mwaminifu na wa haki kwao kama Mungu
wao.”
9 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni: “Ninyi ambao sasa
mnasikia maneno haya yanayozungumzwa
na manabii ambao walikuwepo wakati wa
kuwekwa kwa msingi wa nyumba ya Mwenyezi
Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni,
mikono yenu na iwe na nguvu ili Hekalu liweze
kujengwa.
10 Kabla ya wakati huo, hapakuwa na ujira
kwa mtu wala mnyama. Hakuna mtu aliyeweza
kufanya shughuli yake kwa usalama kwa sababu
ya adui yake, kwa kuwa nilikuwa nimemfanya
kila mtu adui wa jirani yake.
11 Lakini sasa sitawatendea mabaki ya watu
hawa kama nilivyowatenda zamani,” asema
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbin-
guni.
12 “Mbegu itakua vizuri, mzabibu utazaa
matunda yake, ardhi itatoa mazao yake, na
mbingu zitadondosha umande wake. Vitu hivi
vyote nitawapa mabaki ya watu kama urithi wao.
13 Jinsi mlivyokuwa kitu cha laana katikati ya
mataifa, ee Yuda na Israeli, ndivyo nitakavy-
owaokoa, nanyi mtakuwa baraka. Msiogope, bali
iacheni mikono yenu iwe na nguvu.”
14 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni: “Kama
nilivyokuwa nimekusudia kuleta maangamizi
juu yenu, wakati baba zenu waliponikasirisha na
sikuonesha huruma,” asema Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni,

15 “hivyo sasa nimeazimia kufanya mema tena
kwa Yerusalemu na Yuda. Msiogope.
16 Haya ndio mtakayoyafanya: Semeni kweli
kila mtu kwa mwenzake, na mtoe hukumu ya
kweli na haki kwenye mahakama zenu,
17 usipange mabaya dhidi ya jirani yako, wala
msipende kuapa kwa uongo. Nayachukia haya
yote,” asema Mwenyezi Mungu.
18 Neno la Mwenyezi Mungu, Mungu wa ma-
jeshi ya mbinguni likanijia tena.
19 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni: “Saumu ya mwezi wa
nne, ya mwezi wa tano, ya mwezi wa saba, na ya
mwezi wa kumi zitakuwa sikukuu za furaha na
za shangwe kwa Yuda. Kwa hiyo uipende kweli
na amani.”
20 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni: “Mataifa mengi na
wakazi wa miji mingi watakuja,
21 na wenyeji wa mji mmoja wataenda kwenye
mji mwingine na kusema, ‘Twende mara moja
na tukamsihi Mwenyezi Mungu, na kumtafuta
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbin-
guni. Mimi mwenyewe ninaenda.’
22 Pia watu wa kabila nyingi na mataifa
yenye nguvu yatakuja Yerusalemu kumtafuta
Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbin-
guni na kumsihi.”
23 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni: “Katika siku hizo
watu kumi kutoka lugha zote na mataifa,
watang’ang’ania upindo wa joho la Myahudi
mmoja na kusema, ‘Twende pamoja nawe kwa

sababu tumesikia kwamba Mungu yu pamoja nawe.' "

# 9

### *Hukumu juu ya adui za Israeli*

1 Neno la unabii:
Neno la Mwenyezi Mungu liko kinyume na nchi ya Hadraki
na Dameski itakuwa mahali pa kupumzika,
kwa kuwa macho ya watu na ya makabila yote ya Israeli
yako kwa Mwenyezi Mungu;
2 pia juu ya Hamathi inayopakana nayo,
juu ya Tiro na Sidoni,
ingawa wana ujuzi mwingi sana.
3 Tiro amejijengea ngome imara,
amelundika fedha kama mavumbi,
na dhahabu kama taka za mitaani.
4 Lakini Bwana atamwondolea mali yake
na kuuangamiza uwezo wake wa baharini,
naye atateketezwa kwa moto.
5 Ashkeloni ataona hili na kuogopa;
Gaza atagaagaa kwa maumivu makali,
pia Ekroni, kwa sababu
matumaini yake yatanyauka.
Gaza atampoteza mfalme wake
na Ashkeloni ataachwa pweke.
6 Wageni watakalia mji wa Ashdodi,
nami nitakatilia mbali kiburi cha Wafilisti.
7 Nitaondoa damu vinywani mwao,
chakula kile walichokatazwa kati ya meno yao.
Mabaki yao yatakuwa mali ya Mungu wetu,

nao watakuwa viongozi katika Yuda,
naye Ekroni atakuwa kama Wayebusi.
8 Lakini nitailinda nyumba yangu
dhidi ya majeshi ya wanyang'anyi.
Kamwe mdhalimu hatashambulia watu wangu tena,
kwa maana sasa ninawachunga.

### *Kuja kwa Mfalme wa Sayuni*

9 Shangilia sana, ee Binti Sayuni!
Piga kelele, Binti Yerusalemu!
Tazama, Mfalme wako anakuja kwako,
ni mwenye haki, naye ana wokovu,
ni mpole, naye amepanda punda,
mwana-punda, mtoto wa punda.
10 Nitaondoa magari ya vita kutoka Efraimu
na farasi wa vita kutoka Yerusalemu,
nao upinde wa vita utavunjwa.
Atatangaza amani kwa mataifa.
Utawala wake utaenea kutoka bahari hadi bahari,
na kutoka Mto* hadi mwisho wa dunia.
11 Kwako wewe, kwa sababu ya damu ya agano langu nawe,
nitawaacha huru wafungwa wako
watoke kwenye shimo lisilo na maji.
12 Rudieni ngome yenu, enyi wafungwa wa tumaini;
hata sasa ninatangaza kwamba
nitawarejesheeni maradufu.
13 Nitampinda Yuda kama nipindavyo upinde wangu,
nitamfanya Efraimu mshale wangu.

---

* **9:10** yaani *Mto Frati*

Nitawainua wana wako, ee Sayuni,
dhidi ya wana wako, ee Uyunani,
na kukufanya kama upanga wa shujaa wa vita.

### *Mwenyezi Mungu atatokea*

14 Kisha Mwenyezi Mungu atawatokea;
mshale wake utamulika kama radi.
Bwana Mungu Mwenyezi atapiga tarumbeta,
naye atatembea katika tufani za kusini,
15 na Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni atawalinda.
Wataangamiza na kushinda
kwa mawe ya kutupa kwa kombeo.
Watakunywa na kunguruma kama waliolewa mvinyo;
watajaa kama bakuli linalotumika kunyunyizia
kwenye pembe za madhabahu.
16 Mwenyezi Mungu, Mungu wao, atawaokoa siku hiyo
kama kundi la watu wake.
Watang'ara katika nchi yake
kama vito vya thamani kwenye taji.
17 Jinsi gani watavutia na kuwa wazuri!
Nafaka itawastawisha vijana wanaume,
nayo divai mpya vijana wanawake.

## 10

### *Mwenyezi Mungu ataitunza Yuda*

1 Mwombeni Mwenyezi Mungu mvua wakati wa vuli;

ndiye Mwenyezi Mungu atengenezaye
mawingu ya tufani.
Huwapa watu manyunyu ya mvua,
pia mimea ya shambani kwa ajili ya kila mtu.
2 Sanamu huzungumza udanganyifu,
waaguzi huona maono ya uongo;
husimulia ndoto ambazo si za kweli,
wanatoa faraja batili.
Kwa hiyo watu wanatangatanga kama kondoo
walioteseka kwa kukosa mchungaji.

3 “Hasira yangu inawaka dhidi ya wachungaji,
nami nitawaadhibu viongozi;
kwa kuwa Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni
atalichunga kundi lake,
nyumba ya Yuda,
naye atawafanya kama farasi
mwenye kiburi akiwa vitani.
4 Kutoka Yuda litatokea Jiwe la pembeni,
kutoka kwake vitatoka vigingi vya hema,
kutoka kwake utatoka upinde wa vita,
kutoka kwake atatoka kila mtawala.
5 Kwa pamoja watakuwa kama mashujaa
wanaokanyaga barabara za matope
wakati wa vita.
Kwa sababu Mwenyezi Mungu yu pamoja nao,
watapigana na kuwashinda wapanda farasi.

6 “Nitaiimarisha nyumba ya Yuda
na kuiokoa nyumba ya Yusufu.
Nitawarejesha kwa sababu
nina huruma juu yao.

Watakuwa kama watu ambao
sijawahi kuwakataa
kwa sababu mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wao,
nami nitawajibu.
7 Waefraimu watakuwa kama mashujaa,
mioyo yao itafurahi kana kwamba ni kwa divai.
Watoto wao wataona na kufurahi,
mioyo yao itashangilia katika Mwenyezi Mungu.
8 Nitawaashiria na kuwakusanya ndani.
Hakika nitawakomboa,
nao watakuwa wengi
kama walivyokuwa mwanzoni.
9 Ijapokuwa niliwatawanya miongoni mwa mataifa,
hata hivyo wakiwa katika nchi za mbali
watanikumbuka mimi.
Wao na watoto wao watanusurika katika hatari
nao watarudi.
10 Nitawarudisha kutoka Misri
na kuwakusanya toka Ashuru.
Nitawaleta katika nchi ya Gileadi na Lebanoni,
na hapo hapatakuwa na nafasi ya kuwatosha.
11 Watapita katika bahari ya mateso;
bahari iliyochafuka itatulizwa
na vilindi vyote vya Mto Naili vitakauka.
Kiburi cha Ashuru kitashushwa,
nayo fimbo ya utawala ya Misri itatoweka.
12 Nitawaimarisha katika Mwenyezi Mungu,
na katika jina lake watatembea,"
asema Mwenyezi Mungu.

# 11

1 Fungua milango yako, ee Lebanoni,
ili moto uteketeze mierezi yako!
2 Piga yowe, ee msunobari,
kwa kuwa mwerezi umeanguka;
miti ya fahari imeharibiwa!
Piga yowe, enyi mialoni ya Bashani,
msitu mnene umefyekwa!
3 Sikiliza yowe la wachungaji;
malisho yao manono yameangamizwa!
Sikia ngurumo za simba;
kichaka kilichostawi sana
cha Yordani kimeharibiwa!

### *Wachungaji wawili*

4 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu
wangu: "Lilishe kundi lililokusudiwa kuchinjwa.
5 Wanunuzi wake huwachinja na kuondoka
pasipo kuadhibiwa. Wale wanaowauza husema,
'Ahimidiwe Mwenyezi Mungu, mimi ni tajiri!'
Wachungaji wao wenyewe hawawahurumii.
6 Kwa kuwa sitawahurumia tena watu wa
nchi," asema Mwenyezi Mungu. "Nitawakabidhi
kila mtu mkononi mwa jirani yake na mfalme
wake. Wataitenda jeuri nchi, nami sitawaokoa
kutoka mikononi mwao."
7 Kwa hiyo nikalilisha kundi lililotiwa alama
kwa kuchinjwa, hasa kundi lililodhulumiwa
sana. Kisha nikachukua fimbo mbili, moja nikai-
ita Fadhili na nyingine Umoja, nami nikalilisha
kundi.
8 Katika mwezi mmoja nikawaondoa wachun-
gaji watatu.

Kundi la kondoo likanichukia, nami nika-
choshwa nao,
9 nikasema, “Sitakuwa mchungaji wenu.
Waache wanaokufa wafe na wanaoangamia
waangamie. Wale waliobakia kila mmoja na ale
nyama ya mwenzake.”
10 Kisha nikachukua fimbo yangu inayoitwa
Fadhili nikaivunja, kutangua agano nililofanya
na mataifa yote.
11 Likatanguka siku hiyo; kwa hiyo wale
waliodhulumiwa katika kundi, waliokuwa
wakiniangalia wakajua kuwa hilo lilikuwa neno
la Mwenyezi Mungu.
12 Nikawaambia, “Mkiona kuwa ni vyema,
nipeni ujira wangu, la sivyo, basi msinipe.” Kwa
hiyo wakanilipa vipande thelathini vya fedha.
13 Naye Mwenyezi Mungu akaniambia, “Mtupie
mfinyanzi,” hiyo bei nzuri waliyonithaminia!
Kwa hiyo nikachukua hivyo vipande thelathini
vya fedha na kumtupia huyo mfinyanzi katika
nyumba ya Mwenyezi Mungu.
14 Kisha nikaivunja fimbo yangu ya pili iitwayo
Umoja, kuvunja undugu kati ya Yuda na Israeli!
15 Kisha Mwenyezi Mungu akaniambia, “Vit-
wae tena vifaa vya mchungaji mpumbavu.
16 Kwa maana ninaenda kumwinua mchun-
gaji juu ya nchi ambaye hatamjali aliyepotea,
wala kuwatafuta wale wachanga au kuwaponya
waliojeruhiwa, wala kuwalisha wenye afya,
lakini atakula nyama ya kondoo wanono na
kuzirarua kwato zao.
17 “Ole wa mchungaji asiyefaa,
anayeliacha kundi!

Upanga na uupige mkono wake na jicho lake la
kuume!
Mkono wake na unyauke kabisa,
jicho lake la kuume lipofuke kabisa!”

# 12

*Adui za Yerusalemu kuangamizwa*

1 Neno la unabii: Hili ni neno la Mwenyezi
Mungu kuhusu Israeli.

Mwenyezi Mungu, yeye azitandaye mbingu, awekaye misingi ya dunia na aiumbaye roho ya mwanadamu ndani yake, asema:
2 “Nitaenda kufanya Yerusalemu kuwa
kikombe cha kuyumbisha mataifa yote
yanayoizunguka. Yuda utazingirwa kwa vita
na Yerusalemu pia.
3 Katika siku hiyo, wakati mataifa yote ya
dunia yatakapokusanyika dhidi yake, nitau-
fanya Yerusalemu kuwa jabali lisilosogezwa kwa
mataifa yote. Wote watakaojaribu kulisogeza
watajiumiza wenyewe.
4 Katika siku hiyo nitampiga kila farasi kwa
hofu ya ghafula, naye ampandaye nitampiga
kwa wazimu,” asema Mwenyezi Mungu. “Ni-
talielekeza jicho langu la ulinzi juu ya nyumba
ya Yuda, nami nitawapofusha farasi wote wa
mataifa.
5 Kisha viongozi wa Yuda watasema mioyoni
mwao, ‘Watu wa Yerusalemu wana nguvu kwa
sababu Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya
mbinguni ni Mungu wao.’

6 “Katika siku hiyo nitawafanya viongozi wa
Yuda kuwa kama kigae cha moto ndani ya lundo
la kuni, kama mwenge uwakao kati ya miganda.
Watateketeza kulia na kushoto mataifa yote
yanayowazunguka, lakini Yerusalemu utabaki
salama mahali pake.
7 “Mwenyezi Mungu atayaokoa makao ya Yuda
kwanza, ili heshima ya nyumba ya Daudi na
wakazi wa Yerusalemu isiwe kubwa kuliko ile ya
Yuda.
8 Katika siku hiyo, Mwenyezi Mungu
atawakinga wale wanaoishi Yerusalemu, ili aliye
dhaifu kupita wote miongoni mwao awe kama
Daudi, nayo nyumba ya Daudi itakuwa kama
Mungu, kama Malaika wa Mwenyezi Mungu
akiwatangulia.
9 Katika siku hiyo nitatoka kuangamiza mataifa
yote yatakayoshambulia Yerusalemu.

### *Kumwombolezea yule aliyechomwa mkuki*

10 “Nami nitamiminia nyumba ya Daudi na
wakazi wa Yerusalemu roho ya neema* na
maombi. Watanitazama mimi, yule waliyem-
choma. Nao watamwombolezea kama mtu
anayemwombolezea mwanawe wa pekee na
kusikitika kwa uchungu kama anayemsikitikia
mzaliwa wake wa kwanza wa kiume.
11 Katika siku hiyo kilio kitakuwa kikubwa
Yerusalemu, kama kilio cha Hadad-Rimoni katika
tambarare ya Megido.
12 Nchi itaomboleza, kila ukoo peke yake, nao
wake zao peke yao. Ukoo wa nyumba ya Daudi na

* **12:10** au *Roho wa neema*

wake zao, ukoo wa nyumba ya Nathani na wake zao,
13 ukoo wa nyumba ya Lawi na wake zao, ukoo
wa Shimei na wake zao,
14 na koo zote zilizobaki na wake zao.

# 13

*Kutakaswa dhambi*

1 “Katika siku hiyo, chemchemi itafunguliwa
kwa nyumba ya Daudi na wakazi wa Yerusalemu,
kuwatakasa dhambi na unajisi.
2 “Katika siku hiyo, nitayakatilia mbali majina
ya sanamu kutoka nchi, nayo hayatakumbukwa
tena,” asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni. “Nitaondoa manabii wao
pamoja na roho ya uchafu katika nchi.
3 Ikiwa yupo yeyote atakayeendelea
kutabiri, baba yake na mama yake waliomzaa
watamwambia, ‘Ni lazima ufe, kwa sababu
umesema uongo kwa jina la Mwenyezi
Mungu.’ Atakapotabiri, wazazi wake mwenyewe
watampasua tumbo.
4 “Katika siku hiyo, kila nabii ataaibika kwa
maono ya unabii wake. Hatavaa vazi la kinabii
la nywele ili apate kudanganya watu.
5 Atasema, ‘Mimi sio nabii. Mimi ni mkulima;
ardhi imekuwa kazi yangu tangu ujana wangu.’
6 Ikiwa mtu atamuuliza, ‘Majeraha haya yaliyo
mwilini mwako ni ya nini?’ Atajibu, ‘Ni majeraha
niliyoyapata katika nyumba ya rafiki zangu.’

*Mchungaji apigwa, nao kondoo watawanyika*

7 “Amka, ee upanga, dhidi ya mchungaji wangu,
dhidi ya mtu aliye karibu nami!”

asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi
ya mbinguni.
“Mpige mchungaji,
nao kondoo watatawanyika,
nami nitageuza mkono wangu
dhidi ya walio wadogo,
8 katika nchi yote,” asema Mwenyezi Mungu,
“theluthi mbili watapigwa na kuangamia;
hata hivyo theluthi moja watabaki ndani
yake.
9 Hii theluthi moja nitaileta katika moto;
nitawasafisha kama fedha isafishwavyo
na kuwajaribu kama dhahabu.
Wataliitia Jina langu
nami nitawajibu;
nitasema, ‘Hawa ni watu wangu,’
nao watasema, ‘Mwenyezi Mungu ni Mungu
wetu.’ ”

# 14

*Mwenyezi Mungu yuaja kutawala*

1 Siku ya Mwenyezi Mungu inakuja ambayo nyara zilizotekwa kwenu zitagawanywa miongoni mwenu.

2 Nitayakusanya mataifa yote huko Yerusalemu kupigana dhidi yake, mji utatekwa, nyumba zitavamiwa na kuporwa na wanawake watanajisiwa. Nusu ya mji wataenda uhamishoni, lakini watakaobaki hawataondolewa kutoka mjini.

3 Kisha Mwenyezi Mungu atatoka na kupigana dhidi ya watu wa yale mataifa, kama apiganavyo siku ya vita.

4 Siku hiyo miguu yake itasimama juu ya Mlima wa Mizeituni, mashariki mwa Yerusalemu, nao Mlima wa Mizeituni utagawanyika mara mbili kuanzia mashariki hadi magharibi, ukifanya bonde kubwa, nusu ya mlima ukisogea kuelekea kaskazini na nusu kuelekea kusini.
5 Nanyi mtakimbia kupitia katika bonde hilo la mlima wangu kwa kuwa litaenea hadi Aseli. Mtakimbia kama mlivyokimbia tetemeko la ardhi katika siku za Uzia mfalme wa Yuda. Kisha Mwenyezi Mungu, Mungu wangu, atakuja na watakatifu wote pamoja naye.
6 Siku hiyo hakutakuwa na nuru, baridi wala theluji.
7 Itakuwa siku ya kipekee, isiyo na mchana wala usiku, siku ijulikanayo na Mwenyezi Mungu. Jioni inapofika nuru itakuwepo.
8 Siku hiyo, maji yaliyo hai yatatiririka kutoka Yerusalemu, nusu kwenda kwenye bahari ya mashariki*, na nusu kwenda kwenye bahari ya magharibi† wakati wa kiangazi na wakati wa masika.
9 Mwenyezi Mungu atakuwa mfalme juu ya dunia yote. Katika siku hiyo atakuwa Mwenyezi Mungu mmoja, na jina lake litakuwa jina pekee.
10 Nchi yote kuanzia Geba, kaskazini mwa Yuda, hadi Rimoni, kusini mwa Yerusalemu, itakuwa kama Araba‡. Lakini Yerusalemu utainuliwa juu na kubaki mahali pake, toka Lango la Benyamini hadi mahali pa Lango la Kwanza, mpaka kwenye Lango la Pembeni na kutoka

---

* **14:8** yaani *Bahari ya Chumvi* au *Bahari Mfu* † **14:8** yaani *Bahari ya Mediterania* ‡ **14:10** yaani *Nchi tambarare*

Mnara wa Hananeli hadi kwenye mashinikizo ya
divai ya mfalme.
11 Utakaliwa na watu, kamwe hautaharibiwa
tena, Yerusalemu utakaa salama.

12 Hii ndiyo tauni ambayo Mwenyezi Mungu
atapiga nayo mataifa yote ambayo yalipigana
dhidi ya Yerusalemu: Nyama ya miili yao itaoza
wangali wamesimama kwa miguu yao, macho
yao yataoza kwenye matundu yake na ndimi zao
zitaoza vinywani mwao.
13 Katika siku hiyo Mwenyezi Mungu atawatia
wanaume hofu kuu. Kila mwanaume atakamata
mkono wa mwenzake nao watashambuliana.
14 Yuda pia atapigana katika Yerusalemu. Uta-
jiri wa mataifa yote yanayoizunguka Yerusalemu
utakusanywa, wingi wa dhahabu, fedha na
mavazi.
15 Tauni ya aina hiyo hiyo itapiga farasi na
nyumbu, ngamia na punda, nao wanyama wote
walio kwenye kambi za adui.

16 Kisha walionusurika katika mataifa yote
ambayo yaliushambulia Yerusalemu watakuwa
wakipanda Yerusalemu kila mwaka kumwabudu
Mfalme, Mwenyezi Mungu, Mungu wa ma-
jeshi ya mbinguni na kuadhimisha Sikukuu ya
Vibanda.
17 Ikiwa taifa lolote la dunia hawataenda
Yerusalemu kumwabudu Mfalme, Mwenyezi
Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni, mvua
haitanyesha kwao.
18 Ikiwa watu wa Misri nao hawataenda
kushiriki, hawatapata mvua. Mwenyezi Mungu
ataleta juu yao tauni ambayo itayapiga mataifa

ambayo hayataenda kuadhimisha Sikukuu ya
Vibanda.
19 Hii itakuwa adhabu ya Misri na adhabu
ya mataifa yote yale ambayo hayataenda
Yerusalemu kuadhimisha Sikukuu ya Vibanda.
20 Katika siku hiyo, kengele zilizofungwa
kwenye farasi zitaandikwa maneno haya: “Takat-
ifu kwa Mwenyezi Mungu”. Navyo vyungu vya
kupikia katika nyumba ya Mwenyezi Mungu
vitakuwa kama bakuli takatifu mbele ya mad-
habahu.
21 Kila chungu kilicho Yerusalemu na Yuda ki-
takuwa kitakatifu kwa Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni, na wote wanaokuja ku-
toa dhabihu watachukua baadhi ya vyungu hivyo
na kupikia. Katika siku hiyo hatakuwepo tena
mfanyabiashara katika nyumba ya Mwenyezi
Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu
## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d